JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

621 KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA A (GATCE) 2020

## 621 KISWAHILI

*Imechapwa na*:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI ........ iv

1.0 UTANGULIZI ........ 1

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI ........ 2

2.1 Swali la 1: Fasihi ........ 2
2.2 Swali la 2: Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili ........ 4
2.3 Swali la 3: Stadi za Lugha. ........ 7
2.4 Swali la 4: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia ........ 9
2.5 Swali la 5: Sarufi ........ 11
2.6 Swali la 6: Ufundishaji ........ 14
2.7 Swali la 7: Ufahamu ........ 16
2.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia ........ 18
2.9 Swali la 9: Fasihi ........ 20
2.10 Swali la 10: Sarufi ........ 23
2.11 Swali la 11: Fasihi Simulizi ........ 26
2.12 Swali la 12: Utungaji ........ 29
2.13 Swali la 13: Sarufi ........ 31
2.14 Swali la 14: Upimaji katika Kiswahili ........ 34
2.15 Swali la 15: Ufundishaji ........ 37
2.16 Swali la 16: Utungaji ........ 40

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA ........ 43

4.0 HITIMISHO ........ 44

5.0 MAPENDEKEZO ........ 45

*Kiambatisho A* ........ 46

*Kiambatisho B* ........ 47

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili 2020. Uchambuzi umebainisha sababu za watahiniwa kupata alama za juu, wastani au alama hafifu. Aidha, taarifa hii inaonesha sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kufanya vizuri kama vile; kuelewa matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa yaliyofanya waweze kujibu maswali kwa usahihi. Pia, sababu za baadhi ya watahiniwa kupata alama hafifu zimefafanuliwa ikiwa ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa maarifa na kushindwa kujieleza kwa mtiririko wenye mantiki.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho inayoonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kimsingi, majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa maarifa ambayo walipata au walishindwa kupata walipokuwa katika mafunzo ya Ualimu.

Taarifa hii itakuwa nyenzo muhimu kwa viongozi wa elimu, wakufunzi na walimu tarajali katika kupata mbinu sahihi za kuboresha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, wakufunzi wa somo na wengine wote waliohusika kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Charles Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Taarifa hii inachambua ufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Ualimu Daraja la A kwa somo la Kiswahili uliofanyika Mei, 2020 kwa kila swali. Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanyika katika sehemu **A**, **B** na **C.** Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi yalitungwa kutoka katika mada za muhtasari wa *Taaluma* na *Ufundishaji*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote ambapo kila swali lilikuwa na alama nne (4) na kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama arobaini (40). Sehemu B ilikuwa na maswali matatu (3) ya insha ambayo yalihusu mada za *Taaluma* na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali (2) ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Sehemu C ilikuwa na jumla ya maswali matatu (3) ya insha yaliyohusu mada za *Ufundishaji*. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali (2) yenye jumla ya alama kumi na tano (15 kwa kila swali. Kwa ujumla mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali kumi na manne (14) kati ya maswali kumi na sita (16) katika mtihani huu.

Mtihani huu ulikuwa na viwango vitatu vya ufaulu ambavyo ni kiwango kizuri kilichoanzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu kilichoanzia alama 0 hadi 39. Chati za viwango vya ufaulu zimeambatanishwa ili kufafanua viwango vya ufaulu kwa watahiniwa. Rangi ya kijani inawakilisha kiwango kizuri cha kufaulu, rangi ya njano wastani na rangi nyekundu ni kiwango hafifu cha ufaulu.

Jumla ya watahiniwa 3577 walisajiliwa kufanya mtihani wa 621 Kiswahili kwa mwaka 2020. Kati yao, watahiniwa 3536 sawa na asilimia 98.90 walifanya mtihani huu. Aidha, watahiniwa 41 sawa na asilimia 1.14 hawakufanya mtihani. Kiwango cha jumla cha ufaulu cha watahiniwa katika somo hili ni kizuri kwa sababu asilimia 99.91 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walifaulu kwa daraja A hadi D. Kiwango cha ufaulu katika somo hili kwa mwaka 2020 kimeshuka kwa asilimia 0.7 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo asilimia 99.98 ya watahiniwa waliofanya mtihani huo, walifaulu kwa daraja A hadi D.


## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Katika sehemu hii uchambuzi wa takwimu kwa kila swali umefanyika ambapo ufaulu kwa watahiniwa kumegawanyika katika makundi matatu. Mtahiniwa aliyepata kiwango hafifu cha ufaulu alipata kuanzia alama 0 hadi 1.5, kiwango cha wastani cha ufaulu kuanzia alama 2 hadi 2.5 na kiwango kizuri cha ufaulu ni kuanzia alama 3 hadi 4.

### 2.1 Swali la 1: Fasihi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi* na lilimtaka mtahiniwa kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi katika vipengele vya: (a) Umri (b) Uwasilishaji (c) Umiliki na (d) Hadhira.


Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu na lilikuwa ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri, kwani asilimia 95.5 walipata alama za wastani na zaidi. Swali lilikuwa katika ngazi ya kukumbuka na lilihitaji mtahiniwa kueleza vipengele vinavyotofautisha aina za Fasihi. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika swali hili kiasilimia.




**Chati Na. 1:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 91.9 ya watahiniwa waliopata alama za juu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada hii, kwani waliweza kueleza tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kufafanua vipengele vyote. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na


watahiniwa wa kundi hili kuhusu tofauti ya fasihi simulizi na fasihi andishi yalionesha kuwa; *kiumri* fasihi simulizi ni kongwe na fasihi andishi siyo kongwe. Katika *uwasilishaji* walieleza kuwa fasihi simulizi huwasilishwa kwa mdomo na fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi, katika *umiliki* walieleza kuwa fasihi simulizi ni mali ya jamii nzima wakati fasihi andishi ni mali ya mtunzi. Aidha katika kipengele cha *hadhira* walieleza kuwa fanani na hadhira huonana wakati katika fasihi andishi fanani (mwandishi) haonani ana kwa ana na hadhira (wasomaji) wa kazi yake. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa.


1. a) Umri
Fasihi simulizi ni kongwe wakati fasihi andishi sio kongwe.
b) Uwasilishaji
fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo wakati fasihi andishi huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
c) Umiliki
Fasihi simulizi huweza kupotea endapo fanani na hadhira watakufa wakati fasihi andishi huweza kuhifadhiwa kwa muda mrefu kwa sababu huwa katika maandishi.
d) Hadhira
Fasihi simulizi hadhira na fanani huonana ana kwa ana wakati fasihi andishi fanani na hadhira hawawezi kuonana ana kwa ana.

Kielelezo Na. 1.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza tofauti kati ya fasihi simulizi na andishi kwa kuzingatia vigezo vya umri, uwasilishwaji, umiliki na hadhira.

Watahiniwa wachache (4.5%) waliopata alama hafifu walishindwa kutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi katika vipengele vya *Umri, Uwasilishaji, Umiliki* na *Hadhira.* Badala yake walitenganisha vipengele hivyo katika makundi mawili, upande wa fasihi andishi na fasihi simulizi. Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali.



| | |
|---|---|
| 1. Fasihi simulizi | Fasihi andishi |
| b) Uwasilishaji. | a) Umri |
| d) Hadhira | c) Umiliki. |


Kielelezo Na. 1.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na. 1.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza tofauti ya fasihi simulizi na andishi badala yake akaeleza kimakosa kazi za fasihi ambazo ni kuelimisha*, kuburudisha, kuonya na kuimarisha na kuendeleza amali za jamii.*

Watahiniwa wengine (3.6%) walipata alama za wastani ambapo, waliweza kuandika baadhi tu ya majibu yaliyokuwa sahihi kwa kuwa na maarifa ya wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kueleza sifa za fasihi simulizi lakini akashindwa kuzitofautisha na za fasihi andishi.


## 2.2 Swali la 2: Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Uchambuzi wa vifaa vya mtaala wa somo la Kiswahili.* Mtahiniwa alitakiwa abainishe sifa nne muhimu ambazo kitabu cha ziada kinapaswa kuwa nazo. Swali hili ni miungoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na watahiniwa wengi ambapo asilimia 89.4 walipata alama za wastani na zaidi. Chati Na. 2 inafafanua viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 2:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa asilimia 67.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walielewa vizuri mada ya *Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Watahiniwa hao waliweza kueleza sifa tatu hadi nne za kitabu cha ziada kwa hoja kama : *kiwe na maudhui yanayoendana na muhtasari wa somo husika, kinatoa maelezo ya kina juu ya mada zote au baadhi ya mada zilizopo kwenye muhtasari wa somo, kiwe na lugha sanifu na fasaha inayoeleweka kwa wasomaji na kiwe na mazoezi ya wanafunzi ya kutosha.* Watahiniwa wengine waliandika sifa nyingine kama, *kitabu cha ziada kinatakiwa kuwa na utoshelevu wa michoro au picha zinazosadifu mada husika na kuzingatia utamaduni wa jamii husika/kisieleze mambo ambayo ni kinyume na utamaduni wa jamii husika*. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.



2. Sifa za kitabu cha ziada.
i/ Kinatakiwa kuwa na mazoezi ya kutosha.
ii/ Kinatakiwa kiwe kimethibitishwa na taasisi ya elimu.
iii/ Kinatakiwa kuwa na mada zote zinazopaswa kufundishwa
iv/ Kinapaswa kiwe na maarifa ya ziada ambayo hayakuorodheshwa kwenye mtaala.

Kielelezo Na. 2.1 : Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja sifa nne za kitabu cha ziada kutokana na kuelewa matakwa ya swali kwa kuwa na maarifa ya kutosha.

Aidha, asilimia 21.6 ya watahiniwa waliopata alama za wastani waliweza kutaja sifa moja hadi mbili za kitabu cha ziada kama *kuwa na mada zote au baadhi ya mada za muhtasari wa somo, kuwa na michoro ya kutosha, kuwa na mazoezi ya kutosha na pia kiwe kimethibitishwa kuonesha uhalali wa maudhui.*

Watahiniwa wachache, (10.7%) waliopata alama hafifu walishindwa kubainisha sifa nne za kitabu cha ziada. Watahiniwa hao walikosa maarifa katika mada ya vifaa vya mtaala na hasa kipengele cha kitabu cha ziada kama kifaa kimojawapo muhimu cha mtaala. Baadhi ya watahiniwa walichanganya dhana na kutaja sifa za kitabu cha kiada badala ya cha ziada kwa kueleza kuwa ni *lazima kiendane na mtaala, kiwe na ithibati, kiwe na mada kulingana na darasa husika pamoja na muhtasari au kitabu cha mwalimu* na *kuwa na jalada laini na lugha rahisi.* Hata hivyo mtahiniwa mmoja aliweza kueleza kwa usahihi saifa mojawapo tu ya kitabu cha ziada. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha sifa nne muhimu za kitabu cha ziada.



2. a Sifa za kitabu cha ziada
(a) Huwa na Lugha rahisi.
(b) Huwa na jalada Laini.
(c) Huelezea kitu kwa undani zaidi.
(d) Hutumiwa na mwalimu na mwanafunzi katika kujiongezea maarifa zaidi

Kielelezo Na. 2.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.

Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha sifa nne muhimu za kitabu cha ziada kutokana na kukosa maarifa hivyo kuchanganya sifa za kitabu cha ziada na za kitabu cha kiada.


## 2.3 Swali la 3: Stadi za Lugha.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Stadi za Lugha* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika kutambua maandishi pamoja na wepesi wa kusoma kwa kasi. Aidha, mtahiniwa alitakiwa kueleza sifa nne za msomaji mahiri katika usomaji. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni mzuri ambapo asilimia 86.0 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata kuanzia alama 2 hadi 4. Chati Na. 3 inafafanua viwango vya ufaulu kwa asilimia.





**Chati Na. 3 :** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi wa majibu ya watahiwa unaonesha kuwa, asilimia 64.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili vizuri waliweza kueleza sifa za msomaji mahiri kama *vile kuzingatia kasi nzuri ya usomaji, kuzingatia alama za uandishi, kuwa na lafudhi nzuri* na pia msomaji *kutambua maana za maandishi anayosoma*. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.


3. Umahiri wa kusoma ni kitendo cha kuweza kutambua maneno yaliyoandikwa na kuyaelewa. Kuna aina mbili za kusoma kimya na kwa sauti. Zifuatazo ni sifa nne za msomaji mahiri;

Azingatie kasi stahiki ya kusoma; Msomaji mahiri lazima awe na kasi stahiki ya kusoma asisome haraka sana au taratibu sana kwani anaweza kuwachosha wasikilizaji na kushindwa kueleweka vizuri kwa kile anachokisoma.



Azingatie kiimbo; Kiimbo ni kupanda
na kushuka kwa mawimbi ya sauti. Hivyo
basi msomaji mahiri anapaswa azingatie
kiimbo ili kuleta maana sahihi ya neno
alilotamka mfano; barabara. aweke mkazo
parapostahili ili kutopautisha maana na kupeleka.
Azingatie alama za uandishi; Pia
msomaji mahiri anatakiwa kuweza kuzingatia
alama mbalimbali za uandishi kama; koma(,)
au mkato, nukta(.) alama ya mshangao(!) alama
ya kuuliza (?) na funga semi (") funga semi (")
Lafudhi sahihi; msomaji mahiri pia
lazima azingatie awe na lafudhi sahihi ya utamkaji
wa herufi au maneno katika habari anayosoma
lafudhi hutokana na kuathiriwa kwa lugha
mama mfano; kutamka mahalage badala ya
maharage, chakuta - badala ya chakula.
Hivyo basi msomaji mahiri pia anatakiwa
awe anajiamini na mwenye sauti kubwa
inayosikika na kila mtu sauti yenye mvuto.
Ili kuweza kuwavutia wasikilizaji kusikiliza

Kielelezo Na. 3.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Kielelezo Na. 3.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza sifa za msomaji mahiri wa kwa kuwa na maarifa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya Stadi za Lugha.

Watahiniwa wengine, asilimia 21.9 walipata kiwango cha wastani cha ufaulu. Hii ni kwa sababu walikosa maarifa ya kutosha juu ya sifa za msomaji mahiri hivyo kushindwa kupata alama za juu katika swali hili. Watahiniwa hao waliweza kueleza baadhi tu ya sifa za msomaji mahiri kama; kuzingatia alama za uandishi na kuwa na kasi hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 14.0 ya watahiniwa waliopata alama hafifu hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu stadi za lugha. Baadhi ya sifa zisizo sahihi walizozieleza ni kama vile; *msomaji kuwa na msamiati katika lugha, msomaji kuwa na ufahamu na msomaji kuzingatia upatanisho wa kisarufi.* Aidha, watahiniwa wa kundi hili walichanganya maarifa ya dhana mbalimbali za taaluma ya sarufi zisizoendana na Stadi za Lugha. Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kueleza sifa za msomaji mahiri.



3. Msomaji mahiri ana sifa zifuatazo katika usomaji.
(a) Ufahamu, msomaji anatakiwa kuwa na ufah
amu wa kusomo na habari anayoenda kusoma.
(b) Ufasaha, msomaji anatakiwa kusoma kwa
ufasaha kwa kuzingatia kiimbo, kasi statiki,
msamiati na upatanisho wa kisarufi
(c) Utambuzi wa sauti, pia msomaji anapaswa
kuwa na utambuzi wa sauti ambazo ni irab
u na konsonanti.
(d) Msamiati, pia msomaji kuzingatia
misamiati mbalimbali katika lugha.


Kielelezo Na. 3.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza sifa za msomaji mahiri badala yake akaeleza kimakosa dhana zisizohusiana na sifa za usomaji.

## 2.4 Swali la 4: Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia


Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi hasara nne za kutumia mbinu ya masimulizi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi. Swali hili lilitoka katika mada ya Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili

Asilimia 97.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama kuanzia 2 hadi 4 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 88.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada hii. Watahiniwa waliweza kutoa hoja za kutosha zilizokidhi matakwa ya swali. Baadhi ya hoja zilizotolewa ni pamoja na *kupotea au kutumika kwa muda mrefu katika kueleza jambo, wanafunzi kuuliza masawli ambayo hupotosha lengo la somo, wanafunzi kufurahia masimulizi na kushindwa kujifunza lengo mahsusi la somo aidha baadhi ya watahiniwa walieleza kuwa mbinu hii hujenga utegemezi kwa wanafunzi*. Kielelezo Na. 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali.


04 Hasara za Kutumia Mbinu ya masimulizi Kati
ka tendo la ufundishaji na ujifunzaji Kwa
Shule za Msingi

i) Kushindwa Kufikia lengo mahususi. Mbinu
hii hushindwa Kufikia lengo mahususi Kwa
Kutumia muda mwingi Kueleza Kitu Katika
ufundishaji na ujifunzaji.

ii) Kupoteza muda. Muda hupotea Kwa
Kueleza mambo au jambo na wanafunzi Kuuli
za maswali ambayo hupeleke lengo
Mahususi lisifanikiwe Kwa Kurudiarudi masimulizi

iii) Hujenga Utegemezi Kwa Wanafunzi. Kwa
Kufurahia masimulizi hivyo Kushindwa Kuji
funza yeye mwenyewe Kwa Vitendo au Kuten
da.

iv) Huweza Kuleta Ubaguzi au matabaka, Kwa
wanafunzi wenye Usikivu hafifu au Viziwi
Kushindwa Kusikia habari au ujumbe mwalimu
alioukusudia Kufundisha Kwa wanafunzi.


Kielelezo Na. 4.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na maarifa ya kutosha pamoja na kuelewa matakwa ya swali na kuweza

kueleza hasara nne za kutumia mbinu ya *masimulizi* katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi.

Vilevile, asilimia 9.2 ya watahiniwa waliopata kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kueleza baadhi tu ya hasara za kutumia mbinu ya msimulizi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwani walikuwa na maarifa ya wastani juu ya mada hiyo.

Watahiniwa wachache 2.3% walipata alama hafifu kwa kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Baadhi ya majibu waliyoyatoa kimakosa ni kama vile; *kumnyima mwanafunzi fursa ya kujifunza kwa kusoma mwenyewe, kuuwa stadi ya utendaji, kushindwa kukuza udadisi* na *uwezo wa akili ya mwanafunzi huwa mdogo kufikiria.* Kielelezo Na. 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.


4 Hasara 4 za kutumia mbinu ya masimulizi
katika tendo Ufundishaji na Ujifunzaji
i/ Kushindwa kukuza hari ya Udadisi kwa wanafunzi
ii/ Wanafunzi kushindwa kujenga kumbukumbu ya
muda mrefu.
iii/ Mwalimu kutumia maelezo mengi sana wak
ati anafundisha.
iv/ Kuwa stadi ya Utendaji kwa Mwanafunzi

Kielelezo Na. 4.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 4.


Katika kielelezo Na. 4.2 mtahiniwa ameorodhesha hasara za kutumia mbinu ya masimulizi katika tendo la ufundishaji na ujifunzaji badala ya kueleza kwa kifupi mbinu hizo.

## 2.5 Swali la 5: Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi*, kipengele cha sarufi Maumbo (aina za Maneno) katika lugha ya Kiswahili. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika aina za maneno yaliyopigiwa mstari kwa kutumia sentensi zifuatazo: (a) Mtoto mdogo amenunua kiatu kizuri. (b) Mama alimwambia Alfred," Siku zote kaa mbali na mwendawazimu" (c) Lo! Kizuri kimeshanunuliwa. (d) Juma anampenda mchezaji yule. (e) Uvivu wake ulimponza hadi akafukuzwa kazi. (f) Mwalimu aliwahabarisha wanafunzi kuhusu

kufunga shule kwa mwezi mmoja. (g) Dereva alimtoza abiria nauli kubwa. (h) Asalale! Nimesahau kumtumia mama zawadi ya siku kuu.


Asilimia 63.3 ya watahiniwa waliweza kupata kiwango kizuri cha ufaulu katika swali hili kwa kupata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa (45.4%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kubaini aina 2 za maneno. Watahiniwa hao hwakuwa na maarifa ya kutosha juu ya sarufi ya lugha hivyo, kushindwa kubaini aina za maneno katika sentensi.


Asilimia 36.3 ya watahiniwa waliokuwa na kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kubaini aina mbalimbali ya maneno kama yalivyotumika katika sentensi au tungo katika lugha ya Kiswahili. Aidha, walichanganya dhana ya *vivumishi* na *vitenzi*, *nomino* na *vielezi* pamoja na *viwakilishi* katika sentensi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza maana ya maneno hayo badala ya kuonesha aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi kama ifuatavyo; *Nomino ni jina la mtu au mahali*, *Kivumishi ni aina ya neno linalotaja sifa ya jina*, *Kiwakilishi ni maneno yanayochukua nafasi za mahjina katika sentensi*. Kielelezo Na.5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali hili.


5. a) kuandika aina za maneno yaliyopigiwa mstari
a) mtoto mdogo amenunua kiatu kizuri E
(b) mama alimwambia Alfred "siku zote kaa mbali na mwenda wazimu" E
(c) Lo! kiatu kimeshanunuliwa E
(d) Juma anampenda mchezaji yule T
(e) Uvivu wake ulimponza hadi akafukuzwa kazi E
(f) Mwalimu aliwahakikisha wanafunzi kuhusu kufunga shule kwa mwezi mmoja U
(g) Serera alimtoa kauli kubwa

Kielelezo Na. 5.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5.1 sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuandika aina za maneno yaliyopigiwa mstari kwa kukosa maarifa. Watahiniwa hao walichanganya dhana za aina ya maneno kwa kukosa maarifa.

Aidha watahiniwa wachache 18.3% waliopata alama za juu waliweza kubaini aina za maneno kama zilivyotumika katika tungo au sentensi. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kuweza kubaini aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi na kupata alama za juu.


5 a) Kivumishi
b) Nomino
c) Kiwakilishi
d) Nomino
e) Kielezi
f) Kitenzi
g) Kitenzi
h) Kihisishi


Kielelezo Na. 5.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na maarifa ya kutosha hivyo kuweza kubaini aina za maneno yalipigiwa mstari katika sentensi. Aina hizo za maneno ni *Kivumishi, Nomino, Kiwakilishi, Nomino, Nomino Kitenzi, Kitenzi na Kihisishi*.

## 2.6 Swali la 6: Ufundishaji


Swali lilitoka katika mada ya *Ufundishaji* na lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa ya ufundishaji ambapo mtahiniwa alitakiwa *kufafanua kwa* kifupi kazi nne za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa *mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.*

Asilimia 83.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliweza kupata kiwango cha juu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 4. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na. 6:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Asilimia 53.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili waliopata alama za juu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya Ufundishaji pamoja na kuzingatia matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kubaini kazi nne za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Kazi za mwanafunzi zilizobainishwa na kufafanuliwa ni pamoja na *kusikiliza, kujibu maswali, kuuliza maswali, kuandika muhtasari wa maarifa yanayowasilishwa, kuchunguza zana/vielelezo* na *kujadiliana katika makundi.* Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.



6. Kazi nne za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa mapya
i) Kusikiliza kwa makini na kwa utulivu; Mwalimu anapokuwa anawasilisha maarifa mapya mwanafunzi hana budi kukaa kimya na kusikiliza kwa makini anachofundishwa ili kuelewa na kujibu maswali atakayoulizwa.
Kuuliza swali mahala au dhana ambayo hajaielewa na kutolewa ufafanuzi papo kwa hapo na mwalimu wake.
Kujibu maswali kuhusiana na dhana ambayo mwalimu anaiwasilisha kwa namna ambayo yeye anaielewa. Pia kujibu swali atakaloulizwa na mwalimu wake.
Kuandika nukuu ya mambo muhimu ambayo mwalimu anaelezea kuhusiana na dhana au maarifa mapya ambayo mwalimu anawasilisha darasani.
Pia, mwanafunzi anapaswa kushiriki kikamilifu wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo ~~lake~~ husika ili kuweza kumjengea hali ya kujiamini na kupenda somo na kupata kumbukumbu ya muda mrefu.


Kielelezo Na. 6.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na. 6.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini na kufafanua kwa kifupi kazi za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Watahiniwa (29.9%) waliokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu walielewa matakwa ya swali lakini wakakosa maarifa juu ya mada ya Ufundishaji hasa katika kipengele cha kueleza kazi za wanafunzi wakati mwalimu anapokuwa akiwasilisha maarifa mapya.

Watahiniwa wachache (16.9) waliopata alama hafifu walitoa hoja ambazo siyo kazi za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi ya majibu yasiyokuwa sahihi yaliyotolewa na watahiniwa ni pamoja na; *mwanfunzi kuelewa kinachofundishwa, kupokea maarifa, kuwa*

*mdadisi* na *kupokea maarifa yanayowasilishwa na mwalimu.* Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu katika swali hili.



6. (a) kupokea maarifa
(b) kuwa mdadisi juu ya jambo jipyo [illegible]
(c) kuelewa kinachofundishwa
(d) kuwa makini na tulivu

Kielelezo Na. 6.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6.

Kielelezo Na. 6.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubaini na kufafanua kwa kifupi kazi za mwanafunzi wakati mwalimu anawasilisha maarifa mapya katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.


## 2.7 Swali la 7: Ufahamu

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* hususan mada/kipengele cha Ufahamu wa Kusoma na Kusikiliza. Swali lilimtaka mtahiniwa ataje mambo manne ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa. Asilimia 84.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili wamepata kiwango cha juu cha ufaulu kwa kupata alama kati ya 2 hadi 4. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na. 7**: Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia

Uchambuzi unaaonesha kuwa asilimia 51.3 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya Ufahamu wa kusoma na kusikiliza kwani waliweza kubainisha baadhi ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa, baadhi ya mambo yaliyotajwa ni pamoja na *kusikiliza kwa makini, kusoma habari kwa kurudiarudia na kuzingatia matamshi ya msomaji.* Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.



7. i) kusikiliza habari kwa makini.
ii) Kubainisha mawazo makuu au maudhui
iii) Kuzingatia mtiririko wa habari.
iv) Kubainisha ujumbe unaopatikana ktk habari hiy

Kielelezo Na. 7.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa. Mambo hayo ni pamoja na *kusoma au kusimulia kwa kurudia, kubainisha mawazo makuu na kujuamatamshi ya mzungumzaji.*

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 33 ya watahiniwa waliopata alama za wastani waliweza kutaja baadhi ya mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au kusomwa. Baadhi ya hoja sahihi walizoweza kuzitaja ni *kuwa makini kwa kila kinachosimuliwa au kinachosomwa pamoja na kuhusisha mambo muhimu na habari isimuliwayo au inayosomwa.*

Watahiniwa wengine (15.8%) waliopata kiwango hafifu cha ufaulu walishindwa kuelewa misingi na maarifa kuhusu somo la Ufahamu wa Kusoma na Kusikiliza kwani baadhi ya majibu waliyotoa hayana uhusiano wa moja kwa moja na taratibu zinazozingatiwa katika somo la ufahamu wa kusoma na kusikiliza. Kwa mfano, baadhi ya majibu yaliyotolewa kimakosa na watahiniwa kama mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa ni *hali ya hewa nzuri, mazingira tulivu na kukaa kimya*. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili.



7. Mambo ya kuzingatia ili kupata ujumbe katika habari Nyosomwa.
(i) Kukaa kimya
(ii) Kusikiliza kwa makini
(iv) Mazingira tulivu na utulivu
(v) Hali ya hewa nzuri


Kielelezo Na. 7.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutaja mambo manne yanayopaswa kuzingatiwa ili kupata ujumbe katika habari inayosikilizwa au inayosomwa.

## 2.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilitoka katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia na* lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa kifupi tofauti mbili baina ya zana za kufundishia na zana za kujifunzia.


Swali hili ni miungoni mwa maswali ambayo watahiniwa walipata kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kukosa maarifa ya kutosha juu ya tofauti kati ya ya *Zana za Kufundishia* na *Kujifunzia*. Chati Na. 8 inafafanua viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 8:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Asilimia 51.2 ya watahiniwa waliopata alama hafifu katika swali hili walishindwa kueleza tofauti baina ya zana za kufundishia na za kujifunzia kwa kukosa maarifa. Badala ya kutaja tofauti walitaja

kimakosa njia au mbinu zinazotumika kupata zana hizo kuwa ni; *kununua, kukusanya, kuazima, kutengeneza* na *kufaragua*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha totauti baina ya zana za kufundishia na kujifunzia.


8. Tofauti kati ya zana za kufund-ishia na zana za kujifunzia

(i) Zana za kufundishia hutayarishwa moja kwa moja kutoka baraza au kupitia viwandani ~~mfano~~ na wataa-lamu mfano vitabu vya kiada, chaki Muhtasari lakini zana za kujifu-nzia huwezwa kutayarishwa na mwa-afunzi na mwalimu. mfano mpira Tufo

(ii) Zana za kufundishia huwa na gharama kubwa Lakini zana za kujifunzia haina gharama. Kubwa kwa sababu matunzi yake hupatikana katika mazingira.


Kielelezo Na. 8.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.

Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuonesha totauti baina ya zana za kufundishia na kujifunzia kwa kukosa maarifa pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

Aidha, katika swali hili watahiniwa wengi (38.3%) waliopata alama za wastani waliweza kutaja baadhi ya tofauti huku wakichanganya na umuhimu wa zana za kufundisha na kujifunzia kwa kukosa uelewa wa kutosha juu ya mada ya zana za kufundishia na za kujifunzia.

Watahiniwa wachache (10.5%) waliopata kiwango cha juu cha ufaulu wa juu waliweza kutofautisha zana za kufundishia na za kujifunzia. Majibu yaliyotolewa yanaonesha tofauti sahihi baina ya zana za kufundishia na za kujifunzia. Kwa mfano baadhi ya watahiniwa

walieleza kuwa *zana za kufundishia ni kitu chochote ambacho hutumiwa na mwalimu kwa lengo la kurahisisha ufundishaji na huandaliwa na mwalimu.* Wengine walieleza kuwa zana za kujifunzia ni *vitu ambavyo mwanafunzi huvitumia katika ujifunzaji wake na mwanafunzi huweza kuvitumia baada ya mwalimu kuitumia darasani.* Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.



| 8. | Zana za kufundishia | Zana za kujifunzia |
|---|---|---|
| i) | Vifaa ambavyo huvitumia mwalimu anapokuwa anafundisha darasani, mfano picha, vitu halisi na vifani. | Vifaa ambavyo hutumiwa na mwanafunzi ~~na mwalimu~~ katika kukamilisha ujifunzaji wa wanafunzi wenyewe |
| ii) | Mwalimu huviandaa vifaa hivi na kuvitumia kwa kufuata hatua za ufundishaji | Wanafunzi huvitafuta vifaa hivyo na kuweza kuvitumia hata pasipo kuwepo na mwalimu |


Kielelezo Na. 8.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.

Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuonesha totauti baina ya zana na kufundishia na kujifunzia ambazo zipo katika *hatua ya maandalizi, kuchukua nafasi pamoja na muda wake wa kutumika.*

## 2.9 Swali la 9: Fasihi

Swali lilihusu mada ya *Fasihi* katika kipengele cha fasihi andishi ambapo mtahiniwa alitakiwa kuonesha sifa nne za mashairi ya jadi au kimapokeo.

Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu na ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kwa sababu asilimia 91.5 ya watahiniwa walipata alama za juu kuanzia alama 2 hadi 4. Chati Na. 9 inaonesha viwango vya ufaulu katika asilimia.




**Chati Na. 9:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.


Watahiniwa asilimia 82.8 waliopata alama za juu, yaani kuanzia alama 3 hadi 4 kwani waliweza kukidhi matakwa ya swali pamoja na kuweza kubaini au kuonesha sifa za mashairi ya jadi au ya kimapokeo kwa usahihi. Baadhi ya sifa zilizotajwa ni pamoja na *sifa ya kuwa na kibwagizo, mishororo minne kwa kila ubeti, kuwa na vina pia urari wa mizan.* Kielelezo Na.9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vizuri swali hili.

9. Sifa za Mashairi ya jadi

i) huwa na mishororo minne kwa kila beti. Kwa mfano wa beti hii hapa.

Baba ninakulaumu, shule hukunipeleka
Nigelikuwa hakimu, jela ningekupeleka
Ingekufaa hukumu, nyumbani ukaondoka
Mzazi ninakulaumu, shule hukunipeleka

ii) huwa na kibwagizo kwa kila beti. Shairi la kimapokeo huwa na mstari wa mwisho ambao hujirudia kila beti. Mfano wa kibwagizo ni "Mzazi ninakulaumu, shule hakunipeleka".


iii) Huwa na vina vya kati na vya mwisho
mfano katika beti ya hapo juu vina
hivyo ni "Mu" na "ka"


iv) Kila mshororo unamizani kumi na sita
mfano "Ingekufaa hukumu, nyumbani ukaondoka.

Kielelezo Na. 9.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na.9.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza sifa za mashairi ya jadi au kimapokeo ambazo ni *urari wa vina vya kati na vya mwisho, urari wa mizani 16 kwa kila mstari na vipande viwili kila kipande kiwe na mizani nane.*

Watahiniwa wengine (8.8%) waliopata kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kuelewa matakwa ya swali japo walipungukiwa na maarifa na kushindwa kuonesha sifa zote nne za mashairi ya jadi au kimapokeo.

Aidha, asilimia 8.5 ya watahiniwa walipata alama hafifu. Watahiniwa wa kundi hili walishindwa kuelewa mada ya ushairi na hivyo, kuchanganya sifa za mashairi ya jadi na ya kisasa. Vilevile, walieleza dhima za ushairi badala ya sifa za mashairi ya jadi au kimapokeo. Baadhi ya majibu yaliyotolewa ni kama: *Mashairi haya hutumiwa na wanajamii kukosoa, kutoa mafunzo na pia huelimis*ha. Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu.


9 Mashairi ya jadi
i Ni mashairi ambayo hayafuata urari wa vina na beti
ii Hutumiwa na wanajamii katika kukosoa
iii Ina elimisha jamii
iv Hutumika katika kutoa mafunzo

Mashairi ya kimapokeo
i Ni mashairi ambayo hayafuati urari wa vina na beti
ii Ina elimisha jamii
iii Inatumiwa na wanajamii katika sanaa ya muziki
iv Hutumika katika kutoa mafunzo


Kielelezo Na. 9.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza sifa za mashairi ya jadi au kimapokeo kutokana na kushindwa kuelewa matakwa ya swali.

## 2.10 Swali la 10: Sarufi

Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi ya Kiswahili* na lilikuwa na vipengele vinne ambapo mtahiniwa alitakiwa kueleza maana ya istilahi zifuatazo: (a) Kiimbo (b) Shada (c) Silabi (d) Mshangao.


Swali lilijibiwa na asilimia 100 ya watahiniwa waliofanya mtihani. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa sababu asilimia 67.9 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 2 hadi 2.5 na wachache alama za juu, kuanzia 3 hadi 4. Chati Na. 10 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 10:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi unaonesha kuwa asilimia 35.2 ya watahiniwa waliopata kiwango cha juu cha ufaulu waliweza kuelezea kwa usahihi maana ya istilahi zote nne zilizoulizwa katika swali hili. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa ni pamoja na *Kiimbo ni hali ya kupanda na kushuka kwa sauti kutokana na utamkaji wa maneno, Shadda ni mkazo katika utamkaji wa silabi katika maneno, katika Kiswahili shadda huwekwa katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno linalotamkwa, Silabi ni neno au sehemu ndogo ya neno ambayo hutokana na muunganiko wa irabu na konsonanti. Pia zipo silabi zinazotokana na irabu tu mfano a, e, i, o na u na vilevile zipo silabi*

*zinazotokana na konsonanti tu mfano 'm',* Aidha, baadhi ya watahiniwa wameeleza kwa usahihi kuwa *Mshangao* (!) *ni alama inayomwongoza msomaji kubadilii sauti ili kuonesha hisia za maneno yaliyoandikwa*, ambapo yaweza kuwa kushangaa au kushtuka. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.


10. Eleza Maana ya maneno yafuatayo:
a/ Kiimbo
- Ni hali ya kupanda na kushuka kwa sauti inayotokana na utamkaji wa maneno katika binyas.
b/ Shadda.
Ni mkazo wakati wa utamkaji wa maneno shaddah huwababiwa katika kwa kiimbo ambapo neno fulani hutamkwa kwa kukazwa
c/ Silabi
Ni matamshi ya sauti ambapo hupatikana kwa kuunganika irabu na konsonanti
mfano Irabu + Irabu
mfano Konsonanti + Irabu = Silabi
m a ma
d/ Mshangao.
- Ni hali ya alama inayoonyesha kushangaa au kukosea kwa kitu kisichokuwa cha kawaida alama hiyo huonekana !


Kielelezo Na. 10.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza kwa usahihi maana ya *Kiimbo*, *Shada*, *Silabi* na *Mshangao (!)* kwa kuwa waliweza kubaini matakwa ya swali pamoja na kuwa na maarifa ya kutosha.

Watahiniwa wengine 32.7% walipata kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kuweza kueleza dhana moja au mbili za maneno waliyoulizwa.

Watahiniwa hao walipata alama kati ya 2 hadi 2.5 kwani walikuwa na maarifa ya wastani juu ya dhana zilizoulizwa.

Vilevile, asilimia 32.2 ya watahiniwa waliopata alama hafifu walishindwa kueleza maana sahihi ya istilahi za kisarufi katika lugha ya Kiswahili. Wengine walikosa vipengele vyote vya swali na wengine walipata kipengele kimoja tu cha swali hili. Kwa mfano, baadhi ya majibu yaliyotolwa kimakosa katika kuelezea istilahi hizo za kisarufi ni; *Kiimbo ni kupanda na kushuka kwa ala za sauti. Shadda ni kitendo cha kuangalia katika utungaji, Silabi ni muunganiko wa herufi katika neno na sentensi.* Aidha baadhi ya watahiniwa walieleza kuwa *Mshangao* (!) *ni kitendo cha kumtazama mtu au kumwangalia mtu*. Majibu hayo yanadhihirisha kuwa watahiniwa hawakuwa na maarifa juu ya istilahi hizi za kisarufi ambazo hufundishwa katika vipengele mbalimbali vya sarufi hususan sarufi maumbo, miundo na sarufi maana. Kielelezo 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.


10 a) kiimbo ni
Ni kupande ne kushuke kwa ala za sauti.
b Shadda
Ni kitendo cha kuangalia katike utungaji
c Silabi
Ni muunganiko wa herufi katike neno ay sentensi
d Mshangao
Ni kitendo cha kumtazama mtu au kumwangalia
mtu


Kielelezo Na. 10.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10

Kielelezo Na. 10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza kimakosa kuwa, *Kiimbo ni sauti zinazotamkwa kwa midomo ya juu na chini, Shadda ni sauti zinazopanda, Silabi ni mkazo* na *Mshangao* (!) *ni kitendo cha kumshangaa mtu*.

## 2.11 Swali la 11: Fasihi Simulizi

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na lilimtaka mtahiniwa aeleze jinsi methali zinavyoweza kuleta madhara katika jamii iwapo hazitatumika vizuri. Mtahiniwa alitakiwa aoneshe madhara hayo katika vipengele vya: (a) Afya (b) Uchumi (c) Malezi (d) Masuala ya haki na (e) Ushirikishwaji.


Swali lilifanywa na watahiniwa wachache ambao ni asilimia 16.5 ya watahiniwa wote. Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni kizuri ambapo watahiniwa wengi (93.8%) walipata alama za juu kuanzia 3 hadi 4. Chati Na. 11 inafafanua viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 11:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia

Watahiniwa waliopata kiwango cha juu cha ufaulu (53.4%) waliweza kueleza madhara yanaweza kutokea katika jamii iwapo methali hazitatumika vizuri. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha hivyo, kuweza kueleza madhara hayo kwa kutoa mifano ya methali mbalimbali katika vipengele vya *afya, kimalezi, kiuchumi, haki* na *ushirikishaji*. Baadhi ya watahiniwa walitoa mifano kama "*wapishi wengi huharibu mchuzi*". Methali hii inaondoa hali ya ushirikishwaji katika familia au jamii. Aidha methali isemayo "*subira yavuta heri*" katika kipengele cha haki inaweza kusababisha mtu asidai haki yake

ya msingi pale anapodhulumiwa. Kielelezo Na. 11.1: Ni majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa usahihi swali hili.



11 Methali ni kipera cha semi ambacho hutumia lugha ya mafumbo ili kuleta maana kamili au iliyokusudiwa katika jamii. Mfano wa methali ni kuku mgeni hakosi kamba mguuni.

Methali zisipotumika vizuri zinaweza kuleta madhara katika jamii kwenye vipengele vifuatavyo.

Afya. Katika kipengele cha afya methali isipotumika vizuri inaweza kuleta madhara kwa mfano methali ya haraka haraka haina baraka, inaweza kuleta madhara pale ambapo katika jamii au familia atatokea mgonjwa ambae anaumwa sana tusipofanya haraka kumpeleka hospitali anaweza kuzidiwa zaidi au kupoteza maisha.

Uchumi, Katika kipengele cha uchumi methali isipotumika vizuri inaweza kuleta madhara katika jamii kwa mfano methali ya ngombe hanenepi siku ya mnada inaweza kuleta madhara katika jamii kwa kuamini kua matokeo mazuri hayapatikani kwa siku moja hivyo basi itapelekea watu kua nyuma kimaendeleo.

Malezi, katika kipengele cha malezi methali isipotumika vizuri inaweza kuleta madhara katika jamii kwa mfano methali ya asiyefunzwa na mama yake ulimwengu utamfunza methali hii inaweza kuleta madhara katika jamii ambapo humjengea mzazi au mlezi dhana kama mtoto wake anatabia mbaya basi walimwengu na jamii iliyomzunguka itamfunza na wakati anatakiwa ajitahidi kumfunza na kumkanya kwa kile mtoto atakachokua ameenda kinyume ili mtoto asiharibikiwe zaidi. na huwenda walimwengu wasimfunze na akaendelea kua na tabia ile ile.

Masuala ya haki, Katika kipengele cha haki methali zisipotumika vizuri zinaweza kuleta madha

Kielelezo Na. 11.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.1: Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi kwa kuonesha madhara ya methali katika vipengele vya: (a) Afya (b) Uchumi (c) Malezi (d) Masuala ya haki na (e) Ushirikishwaji.

Watahiniwa waliopata kiwango cha wastani cha ufaulu (40.5%) waliweza kueleza hasara za methali moja au zaidi hivyo, kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya wastani hivyo kuweza kueleza hasara hizo katika baadhi tu ya vipengele vya swali.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama hafifu hawakuwa na maarifa pamoja na kushindwa kujua matakwa ya swali hivyo, kueleza mifano ya methali zinazosawiri madhara ya methali pale zinapotumika vibaya. Maelezo yaliyotolewa na watahiniwa hayakuonesha jinsi gani methali hizo zinaweza kuleta madhara iwapo zitatumika vibaya badala yake walieleza faida au umuhimu wa methali walizochagua. Mfano, katika kipengele cha Uchumi, methali ya *'Mchumia juani hulia kivulini'*. Mtahiniwa alieleza kimakosa faida yake badala ya hasara kuwa husisitiza kujituma kufanya kazi na matunda yake hupatikana baadaye. Vilevile, methali kama '*Mchelea mwana kulia hulia yeye',* mtahiniwa alieleza kimakosa kuwa methali hii inasisitiza kuwa, kama mwanamke anaonewa anapaswa kushtaki mapema ili kupata haki zake. Maelezo haya yanaonesha umuhimu wa methali hiyo kwa anayeonewa na si madhara. Kielelezo Na. 11.2: ni sapuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.


11: Methali ni misemo ambayo hutolewa kwa mafumbo. Zifuatazo ni namna ambavyo methali zisipotumika vizuri zinaweza kuleta madhara katika jamii:

Afya, kwa mfano methali ya Hakuna mauka, yasiyokuwa na mbu, methali hii isipotumiwa vizuri inaweza kuleta madhara kwa watu kwa kujipuuzia na kupata magonjwa kama malaria.

Malezi, mfano Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo, methali hii ikitumika vibaya inaleta madhara maana mtoto ulimdekezo anashindwa atakufanya kazi.

Ushirikishwaji, mfano Fuata nyuki ule asali methali hii hushirikisha kwa kufanya kila jambo mfano kazi tufanye kwa pamoja wanawake na wanaume.

Uchumi, mfano mchumia juani ulia kivuli ni, methali hii hutujengea uchumi kwa kujituma kufanya kazi kwani matunda yake tutapata baadae.



Masuala ya haki, mfano mchelea mwana
kulia hulia yeye, methali hii hutukumbusha kuwa kama
mwanamke anaonewa anapaswa kulitaki mapema ili
kupata haki zako.
Hivyo basi yote hapo juu ni methali ambazo
zisipotumika vizuri huleta madhara.


Kielelezo Na. 11.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama hafifu kwa kuonesha umuhimu wa methali badala ya madhara katika vipengele vya: (a) Afya (b) Uchumi (c) Malezi (d) Masuala ya haki na (e) Ushirikishwaji kwa kukosa maarifa pamoja na kushindwa kujua matakwa ya swali

## 2.12 Swali la 12: Utungaji


Swali lilitoka katika mada ya *Utungaji* na lililenga kupima uwezo wa mtahiniwa wa kuandika barua za kikazi/kiofisi. Mtahiniwa alitakiwa kuandika barua kwa Afisa Elimu kumweleza kuhusu upungufu wa vitabu vya kiada vya somo la Kiswahili.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri zaidi kwani asilimia 99.9 ya watahiniwa waliojibu swali walipata kuanzia alama 6 hadi 15. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na. 12:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa (81.9%) waliopata alama za juu katika swali hili waliweza kuandika kwa usahihi barua ya kikazi/kiofisi kwa kuzingatia vipengele vya barua. Vipengele hivyo ni pamoja na *anwani ya mwandikiwa, tarehe, kumbukumbu namba ya barua na mwishoni jinsi ya kuweka saini na jina la mwandishi*. Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.



12.

SHULE YA MSINGI MTINIKWETU,
S. L. P 75,
NACHINGWEA.
30/6/2020.

AFISA ELIMU,
S. L. P 220,
NACHINGWEA.

Ndg,

YAH: UPUNGUFU WA VITABU VYA KIADA VYA SOMO LA KISWAHILI.

Kichwa cha habari hapo juu chahusika. Mimi ni mwalimu katika shule ya msingi Mtinikwetu iliyopo wilaya ya Nachingwea.

Shunani la kuandika barua hii ni kukutaarifu kuwa tuna upungufu wa vitabu vya kiada ya somo la kiswahili.

Ni matumaini yangu kuwa utapokea ujumbe taarifa hii na kuishughulikia.


Wako katika ujenzi wa taifa,
Barali.
Mwalimu Mary.

Kielelezo Na. 12.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 12.

Kielelezo Na. 12.1: kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kuandika vizuri barua ya kiofisi kwa kuzingatia utaratibu wa uandishi sahihi wa barua ya kiofisi/kikazi.

Watahiniwa (18.0%) waliopata alama za wastani walishindwa kuandika baadhi ya vipengele muhimu katika uandishi wa barua za kiofisi. Kwa mfano, wapo walioshindwa kuonesha kiusahihi mpangilio wa *anwani ya mwandikiwa, tarehe inapoandikwa, kumbukumbu namba ya barua na mwishoni jinsi ya kuweka saini na jina la mwandishi*. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu

ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kushindwa kuandika kwa usahihi barua ya kiofisi kwa kuzingatia utaratibu wa uandishi sahihi.



2.

Shule ya msingi Mtinikawefu,
S.L.P 940,
Nachingwea,
30/06/2020.

Afisa Elimu,
Nachingwea,

YAH: UPUNGUFU WA VITABU VYA KIADA SOMO LA KISWAHILI.

Husika na mada tajwa hapo juu. Mimi ni mwalimu wa shule ya msingi Mtinikawefu katika wilaya ya Nachingwea, Ni mwalimu wa somo la kiswahili katika shule hii, Nakutaarifu kuwa kuna upungufu mkubwa wa Vitabu vya somo la Kiswahili ampapo inapelekea somo hili kutokuendelea Vizuri kitaaluma kwa kukosa Vipaa hivi muhimu vya kufundishia. Hivyo naomba unipatie Vitabu hivyo ili ufundishaji uweze kuendelea Vizuri.

Naamini ombi langu litakubaliwa.

Wako mtiifu katika kazi.
Mwlm. Zulfa.


Kielelezo Na. 12.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za wastani kwa kushindwa kuandika barua ya kiofisi kwa kuzingatia utaratibu wa uandishi sahihi.

## 2.13 Swali la 13: Sarufi


Swali lilitoka katika mada ya *Sarufi* kipengele cha kauli ya utendaji ambapo mtahiniwa alitakiwa abainishe aina tano za kauli za utendaji katika lugha ya Kiswahili kwa kutumia mifano.

Asilimia 98.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama kuanzia 6 hadi alama 15. Watahiniwa wachache (1.3%) walipata alama hafifu hivyo kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati namba 13 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 13:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa (80.5%) walipata alama za juu kuanzia alama 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Sarufi* hususan kauli za utendaji. Watahiniwa waliweza kubaini kauli tano za utendaji na kutoa mifano sahihi. Kauli hizo ni pamoja na *kauli ya kutenda*, *kauli ya kutendwa*, *kauli ya kutendewa*, *kauli ya kutendeka*, *kauli ya kutendea na pia kauli ya kutendana*. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali kwa usahihi.




13 Kauli ya utendaji ni kauli zinazoonyesha namna au jinsi kitu fulani kilivyofanyika au Namna ya jinsi kitu fulani kilivyo. Zifuatazo ni aina za kauli za utendaji.

Kauli ya Kutendwa, Kauli hii huonyesha jinsi jambo fulani lilivyofanywa mfano "Mti umekatwa" inaonyesha mti ulivyotendwa. kitendo ni kata na mti umekatwa.

Kutenda, Mfano Imba wimbo, ni kauli ya kutenda yaani kuimba ambapo kitendo ni kuimba na kutenda ni kuimba wimbo.

Kauli ya Kutendewa Mfano wimbo Umeimbwa nini ni kauli inayoonyesha kwa Kilichotendewa ni wimbo kwa kuimbwa.




Kauli ya Kutendeka, Mfano wimbo Umeimbika vizuri, Hii ni kauli inayoonesha namna wimbo ulivyopangika ulivyoimbwa.
Kauli ya Kutendeana Mfano Imbiana, Pigana, rushiana, umizana hii ni Mifano ya kauli ya kutendeana.
Kauli ya Kutendea mfano Imbia Limia, pigia, hii ni utenzi unaoonyesha kauli ya kutendea.
Kwa ujumla kauli zote za utendaji hutokana na kauli taarifa na kauli halisi katika kuzungumza lugha yoyote.

Kielelezo Na. 13.1: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 13.

Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha kauli mbalimbali za utendaji katika sentensi.

Watahiniwa (18.1%) walipata alama za wastani kuanzia alama 6 hadi 10 kwa kushindwa kutimiza matakwa ya swali. Baadhi waliweza kubaini kauli za utendaji bila kuonesha mifano na wengine hawakuweza kubainisha aina zote tano kama swali lilivyotaka.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa wachache (1.3%) walipata alama hafifu kwa kushindwa kuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza dhana ya *kauli za utendaji, kusoma, kuandika, mpangilio wa mawazo na suala la ufupisho katika uandishi wa habari* badala ya kuainisha aina za kauli ya utendaji katika lugha ya Kiswahili. Hii inaonesha kuwa, mtahiniwa hakuelewa matakwa ya swali pamoja na kukosa maarifa. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.


13 Lugha ni sauli za nasibu iliyokubaliwa katika jamii fulani ili iweze kuhimilka katika mawasiliano. Yafuatayo ni aina tano za kauli ya utendaji katika lugha ya Kiswahili
Lugha rahisi na inayoeleweka kwa watu wote; ili waweza kuelewa ujumbe mbali mbali ipasavyo
Kusoma; mtu alitaka kuwasilisha ujumbe katika jamii fulani anapaswa kujua kusoma ili ujumbe huo uwezo kufika katika jamii husika.
Kuandika; ili utendaji katika lugha ya kiswahili uweze kuwasilishwa katika jamii fulani inapaswa kuandikwa kwa mtiririko mzuri.
Mawazo makuu; hii ni mojawapo katika kauli ya utendaji wa lugha ya kiswahi mtu yeyote anapaswa kubaini mawazo makuu inayompelekea kupata taarifa iliyo kamili katika wazo hilo.
Mpangilio mzuri wa mawazo ili watu wote waweze kutumia lugha hiyo au wazo hilo ipangwe katika mpangilio mzuri ili mtu yeyote aweze kuwasilisha ujumbe huo katika jamii husika.
Kwa hiyo basi kauli ya utendaji katika lugha ya kiswahili ni muhimu kwa sababu huweza kufupisha habari, kukuza vipaji mbalimbali na huweza kufuata kanuni mbalimbali za uandishi na kufikisha ujumbe kwa wakati katika jamii husika.


Kielelezo Na. 13.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.

Kielelezo Na. 13.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza kauli tano za utendaji katika lugha ya Kiswahili.

## 2.14 Swali la 14: Upimaji katika Kiswahili

Swali lilitoka katika mada ya *Upimaji katika Somo la Kiswahili* na lilimtaka mtahiniwa kufafanua aina sita za maswali yanayotumika kumpima mwanafunzi wa Shule za Msingi kwa kutoa mifano.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 96.8 ya watahiniwa waliojibu swali walipata alama kuanzia 6 hadi alama 15. Chati Na. 14 inaonesha viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 14:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Watahiniwa (54.5) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia alama 6 hadi 10 kwani walikuwa na uelewa wa wastani. Watahiniwa wengi waliainisha aina sita za maswali yanayotumika bila kutoa mifano. Aidha, wapo waliotoa maelezo tofauti na matakwa ya maswali hayo. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitaja *maswali ya maelezo na maswali ya insha* kwa kumaanisha kuwa ni aina tofauti za maswali.Vilevile baadhi ya watahiniwa waliweza kueleza kufafanua aina za maswali lakini wakashindwa kutoa mifano hivyo, kupata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, watahiniwa (42.3%) waliweza kujibu swali hili vizuri na kupata alama za juu kuanzia alama 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada hii. Watahiniwa hawa waliweza kubainisha aina za maswali na kutoa mifano sahihi. Aina ya maswali yaliyobainishwa na watahiniwa katika kundi hili ni pamoja na *maswali ya kuandika kweli au si kweli*, *maswali ya kuoanisha*, *maswali ya kuchagua jibu sahihi*, *maswali yanayohitaji majibu mafupi*, *maswali ya kujaza nafasi zilizo wazi na pia mswali ya insha*. Kielelezo Na.14 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata kiwango cha juu cha ufaulu.


14 Maswali ni nyenzo au vifaa anavyotumia mwalimu katika mchakato mzima wa upimaji. Maswali haya yana tumika katika kufanya tathimini ya somo yaani kufi kiwa kwa malengo mahususi. yafuatayo ni aina ya maswali yanayotumika katika kupima shule za msingi

Maswali ya kuchagua jibu sahihi; haya ni maswali yanayotumika kupima uwezo wa kufikiri au kukumbuka ambapo yanahitaji jibu lililosahihi ambapo swali la kuchagua jibu sahihi huwa na majibu zaidi ya mawili na kuendelea mfano wa swali la kuchagua jibu sahihi Bendera ya Tanzania ina rangi ngapi? a) 2 b) 3 c) 4 d) 5 (4)

Maswali ya kweli au si kweli; ni aina ya maswali ambayo majibu yake lazima yiandike kweli au si kweli ambapo yanamtaka mwanafunzi kuchagua jibu la kweli au si kweli mfano Tanganyika ilipata uhuru mwaka 1961 kweli.

Maswali ya kuoanisha haya ni maswali ambapo huwa na pande mbili yaani A na B ambapo pande hizi mbili upande mmoja huwa na swali pia upande mwingine huwa na majibu ambapo majibu huwa mengi kuliko maswali pia hupima mada moja mfano oanisha sentensi zifuatazo kipengele A: kitenzi B) aina za maneno

Maswali ya kuacha nafasi wazi, haya ni maswali ambayo yanahitaji ambapo mwalimu hutunga swali na kuacha nafasi wazi ili mwanafunzi aweze kujaza mfano wa swali la kujaza nafasi wazi kuna aina ngapi za maneno? 7. ambapo mwanafunzi hutakiwa kujaza nafasi hiyo wazi ili kukamilisha sentensi katika swali



Maswali yanayohitaji maelezo mafupi. Haya ni maswali ambayo huhitaji maelezo mafupi katika kujibu ambapo mwanafunzi hutakiwa kutoa maelezo mafupi katika kifungu cha habari mfano katika kusoma habari kisha kueleza habari ili kuwa inahusu nini.

Maswali ya Insha. Haya ni maswali ambayo mwalimu ~~au~~ anaweza kutunga Insha au kuwaambia wanafunzi kutunga Insha kuhusiana na jambo fulani au mwalimu kuwasomea kifungu cha habari Insha kisha wanafunzi wanaandika.

Kwa kuhitimisha Umuhimu wa maswali inasaidia kujua maendeleo ya mwanafunzi na matatizo au changamoto katika ujifunzaji wake kupitia maswali pia inasaidia kufanya tathimini ya somo.


Kielelezo Na. 14: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 14.

Kielelezo Na.14 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufafanua aina sita za maswali yanayotumika kupima wanafunzi na kupata ufaulu wa juu.

## 2.15 Swali la 15: Ufundishaji


Swali lilitoka katika mada ya *Ufundishaji kipengele cha Shajara la somo* na lilikuwa na vipengele viwili, ambavyo vilimtaka mtahiniwa (a) Kueleza maana ya Shajara la somo na (b) Mtahiniwa alitakiwa kufafanua vipengele vinne vya Shajara la somo la Kiswahili.

Asilimia 98.02 walipata alama za wastani kwa kupata alama 6 hadi 15 hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha juu cha ufaulu. Chati Na.15 inaonesha kiwango cha ufaulu katika asilimia.





**Chati Na. 15:** Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 55 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata kiwango cha juu cha ufaulu kwa kupata alama kuanzia 10.5 hadi 15. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada kwani waliweza kueleza maana ya shajara la somo na kufafanua vipengele vyake. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja vipengele vya shajara la somo kuwa ni *dhana /ujuzi unaofundishwa*, *maoni ya mkuu wa idara*, *taarifa za jumla* na *tarehe ya kuanza* na *kumaliza*. Kielelezo Na.15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili na kupata alama za juu.


15 b) (i) Dhana/ujuzi uliofundishwa ni kipengele cha shajara ambacho kinaonyesha vitu vyote vilivyofundishwa kwa kuanzia na mada kuu yenyewe Mada ndogo na vipengele vidogo vidogo vilivyotokana na mada ndogo zote kwa kila mada kuu fulani hadi kuhakikisha kwa mada fulani na dhana au ujuzi fulani uliofundishwa kupitiwa.

ii) Maoni ya Mkuu wa Idara.
- Maoni haya huandikwa katika ukurasa wa Sahihi au maoni ambapo Mkuu wa Idara huandika maoni yake baada ya mwalimu husika mwenye somo ni aliyefundisha huandika maoni yake. Mkuu wa Idara huandika maoni kulingana na mada fulani na jinsi ambavyo mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unavyoendelea.


iii/ Taarifa za jumla/Awali:
Sehemu au kipengele hiki cha shajara hubeba vitu vingi mfano, Jina la shule, jina la mwalimu, Somo, darasa, muhula ambapo hujazwa na kukamilishwa na mwalimu wa somo anayeandaa shajara hilo.
Sehemu hii huwa ni taarifa za jumla au za awali kwa kuwa ndiye sehemu hapo mtu huona aina ya walengwa yaani darasa fulani na jina la mwalimu ili mwalimu aweze kutambulike
use only
15(b) iii Wakati wa ukaguzi.
iv/ Tarehe ya kuanza na kumaliza.
Kipengele hiki ni muhimu kukamilisha na ndio hubeba maana halisi ya shajara la somo.
Tarehe ya kuanza hujazwa pale ambapo mwalimu anaanza rasmi kufundisha mada husika na
Tarehe ya kumaliza hujazwa siku ambayo mwalimu amemaliza kufundisha mada fulani.
Hivyo sehemu/kipengele huwaidia kupima kasi ya ufundishaji ya mwalimu.

Kielelezo Na.15.2: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 15.

Kielelezo Na.15.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza dhana ya shajara la somo pamoja na kufafanua vipengele vyake.


Vilevile, asilimia 42.5 ya watahiniwa waliopata kiwango cha wastani cha ufaulu waliweza kujibu baadhi tu ya maswali na kupata alama kuanzia 6 hadi alama 10. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya wastani kuhusu *Shajara la Somo* kama kipengele muhimu sana kwa mwalimu anayefundisha darasani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kuwa, *Shajara la Somo ni Muhtasari unaoonesha mada zitakazofundishwa na idadi ya maswali katika kila nyanja na ngazi zake.* Kwa ujumla watahiniwa katika kundi hili walikuwa na uelewa

wa wastani katika mada hii, hivyo waliweza kueleza baadhi tu ya hoja zinazohusiana na shajara za somo na kushindwa kufafanua vipengele vyake kulingana na matakwa ya somo.

## 2.16 Swali la 16: Utungaji

Swali lilihusu mada ya *Utungaji katika kipengele cha ufupisho* na lilimtaka mtahiniwa aeleze hatua sita za kufuata wakati wa kufundisha somo la ufupisho kwa wanafunzi wa darasa la Saba.

Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vibaya ambapo (2.4%) tu ndio walipata alama 10.5 hadi 15. Chati Na. 16 inafafanua viwango vya ufaulu kwa asilimia.




**Chati Na. 16**: Ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa waliopata alama za chini (56.7%) hawakuelewa matakwa ya swali hivyo, walieleza *dhana ya ufupisho* badala ya hatua za kufundisha somo la ufupisho. Aidha, wapo waliotaja kimakosa hatua hizo kuwa ni *ufahamu kama hatua ya kwanza, ubainishaji wa matumizi ya lugha na kanuni za uandishi na mwishoni kutoa kazi ya kufanya ufupisho.* Kielelezo Na. 16.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali.

16. Kueleza hatua 6 (sita) za kufuata katika kufundisha somo la Ufupisho wa wanafunzi wa Darasa la saba.

(I) Nitawaongoza wanafunzi katika kujua neno / istilahi ya neno Ufupisho nini kwanza. Ufupisho. Ni kitendo cha kufupisha maneno katika ukurasa wa mada uliosomwa kwa kubaini malengo muhimu katika mada hiyo

(II) Nitawaongoza wanafunzi baada ya kujua maana ya Ufupisho, kufahamu hatua zinazofuata kwenye ufupisho.

(III) Nitaorodhesha hatua moja hadi nyingine kwa kuelezea na kutoa ufafanuzi wakina.

- Soma habari na uielewe vizuri
- Baini matumizi ya lugha na kanuni za uandishi.
- Kisha andika kwa ufupi kutokana na kile ulichokisoma kwa kubaini vitu muhimu vilivyopo kwenye habari.
- Baada ya kufupisha urefu huo wa habari.
- Rudia tena kuisoma habari hiyo.

(IV) Baada ya kumalizia nitatoa zoezi dogo kwa wanafunzi kufanya ufupisho wa kitabu cha Hadithi ili kupima uelewa wao katika kujifunza mada ya Ufupisho.

Kielelezo Na. 16.1: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 16.

Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza hatua za kufuata katika kufundisha somo la ufupisho kwa mpangilio maalum.

Aidha asilimia 40.9 ya watahiniwa walipata kiwango cha wastani cha ufaulu kwani waliweza kueleza hatua za kufundisha ufupisho

lakini wakashindwa kutaja hatua hizo kwa mtiririko maalum. Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza hatua za ufupisho kwa kufuata mpangilio maalum.

16. Ufupisho ni kitendo cha kusoma matini au kusikiliza habari fulani na kuweza kuelewa vizuri na kuifupisha bila kupoteza ujumbe au maana ya taarifa hiyo. mfano Unaweza kusoma habari katika kitabu na kuweza kuifupisha bila ya kupoteza maana ya habari hiyo. Katika ufundishaji wa ufupisho kuna hatua za kufuata nazo ni kama ifuatavyo.

Kuandaa kifungu cha habari mwalimu anaweza kuchagua kifungu cha habari kutoka katika vitabu vyao au kutoka katika matini mbalimbali ambazo zinaeleza maudhui yanayoendana na umri wa wanafunzi wake. mfano matini au kifungu hicho kinaweza kueleza namna ya kuhifadhi mazingira ya nyumbani.


Kuwasomea wanafunzi kifungu hicho cha habari huku wanafunzi wakisikiliza kwa makini ili kujua habari inazungumzia kitu gani. pia kama kuna uwezekana mwalimu anaweza kuandika kifungu hicho cha habari katika karatasi na kumgawia kila mwanafunzi asome mwenyewe.

Kubaini mawazo makuu katika kila aya ya kifungu cha habari hiyo. Ikiwa kifungu kina aya zaidi ya moja basi mwanafunzi anapaswa kubaini mawazo kutoka katika kila aya.

Kuunganisha mawazo makuu yaliyotoka katika kila aya kwa kutumia msamiati inayojitosheleza ili kuzuia uwezekano wa kutumia maneno mengi.

Kufupisha habari kulingana na idadi ya aya au maneno uliyopewa. mfano habari iliyokua na maneno 300 unaambiwa ufupishe habari hiyo katika maneno 200.

Kuhakiki idadi ya maneno yaliyoagizwa kwa kuhesabu neno moja moja na kusoma habari yako uliyofupisha kama inaleta maana iliyokusudiwa kama mwanzoni kabla ya kufupisha.



Hivyo basi ufupisho humjengea mwan
afunzi uwezo wa kuandika pia humj
engea ufikirishaji kwani anavyoweza
kubaini wazo kuu kwa kila aya -
kutumia akili kuchanganua mambo ya
msingi na ya muhimu yaliyo katika -
habari hiyo.

Kielelezo Na. 16.2: Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 16.

Kielelezo Na. 16.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza hatua za kufuata katika kufundisha somo la ufupisho kwa wanafunzi wa Darasa la Saba katika mtiririko maalum.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU KWA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa 621 Kiswahili ulikuwa na maswali (16) yaliyotoka katika mada 10. Mada hizo ni *Utungaji, Upimaji katika somo la Kiswahili, Uchambuzi wa vifaa vya Mtaala, Fasihi Simulizi, Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia somo la Kiswahili, Stadi za Lugha, Ufahamu na Sarufi Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili na Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Kiswahili*. Mada mbili zilizokuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili na Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la Kiswahili.*

Uchambuzi wa kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mada unaonesha kuwa, watahiniwa wamefanya vizuri katika mada 8. Mada hizo ni *Utungaji (99.9%), Upimaji katika Somo la Kiswahili (97.2%), Fasihi Simulizi (94.7%), Uchambuzi wa vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili (93.7%), Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili (90.4%), Stadi za Lugha (86%), Ufahamu (84%) na Sarufi* (76.8%) ambazo ni sawa na asilimia 80 ya mada zilizotahiniwa. Watahiniwa walipata kiwango kizuri cha ufaulu katika mada zilizotajwa kwa sababu waliweza kujieleza vizuri kwa lugha inayoeleweka, kujenga hoja vizuri katika mtiririko unaoleta mantiki pamoja na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hususan katika maswali ya insha.

Aidha, watahiniwa wamepata kiwango cha wastani cha ufaulu katika mada 2 ambazo ni *Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili (48.8)* na *Maandalizi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili (43.3).* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa wastani wa mada hizo, hivyo kushindwa kujibu maswali kikamilifu pamoja na kufuata kanuni za uandishi katika maswali ya insha kama ilivyofafanuliwa katika Kiambatisho A.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2019 ulikuwa asililimia 99.98 ambapo jumla ya mada 8 zilitahiniwa. Aidha jumla ya mada 10 zilitahiniwa katika mtihani wa mwaka 2020 ambapo kiwango cha ufaulu ni 99.91. Kwa ujumla kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2020 kimeshuka kwa asilimia 0.7 ukilinganishwa na mwaka 2019 kama inavyoonekana katika Kiambatisho B.

## 4.0 HITIMISHO

Mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2020 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Kiswahili pamoja na Nyanja ambazo ni utambuzi, maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini. Kiwango cha ufaulu kwa ujumla kilikuwa kizuri kwa kuwa zaidi ya theluthi mbili ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

Sababu zilizofanya baadhi ya watahiniwa kushindwa kufanya vizuri baadhi ya mada zimebainishwa. Changamoto hizo ni; Kushindwa kuelewa matakwa ya swali, kukosa maarifa na kushindwa kuandika insha zenye mtiririko unaoleta mantiki. Aidha, baadhi ya watahiniwa waliweza kujibu maswali lakini wakalishindwa kutoa mifano sahihi kwa majibu waliyotoa.

Ni matarajio ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa, wakufunzi na walimu tarajali wa somo hili, watatumia changamoto zilizobainishwa kufanya maboresho yatakayowezesha kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu hasa katika mada zilizokuwa na kiwango cha wastani. Aidha, wakufunzi watatumia changamoto hizo kama fursa ya kuandaa mazingira bora zaidi ya kuwafundisha walimu tarajali ili kupata stadi na maarifa ili kuimudu lugha adhimu ya Kiswahili.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Mambo yafuatayo yanapendekezwa ili kuinua kiwango cha ufaulu katika somo hili:

(a) Ufundishaji na ujifunzaji katika mada za Zana za Kufundishia na Kujifunzia na Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili ufanyike kwa njia shirikishi ili kuwajengea walimu tarajali uwezo wa kubaini tofauti kati ya zana za kufundishia na zana za kujifunzia.

(b) Wakufunzi wawaandalie walimu tarajali mazoezi ya ufundishaji kiduchu ya mara kwa mara ili kuwajengea umahiri wa kufundisha mada ya Utungaji hususani mada ndogo ya *Ufupisho*.

(c) Aidha, Walimu tarajali wapewe mazoezi ya kutosha ili kuwajengea uwezo wa kubaini matakwa ya swali na kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

*Kiambatisho A*

## MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA KISWAHILI

| Na. | Mada | Namba ya swali | Ufaulu Katika Kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu Katika Kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Utungaji | 12 | 99.9 | 99.9 | Vizuri |
| 2. | Upimaji katika somo la Kiswahili | 14 | 97.2 | 97.2 | Vizuri |
| 3. | Fasihi Simulizi | 1 | 98.7 | 94.7 | Vizuri |
| | | 9 | 91.5 | | |
| | | 11 | 93.8 | | |
| 4. | Uchambuzi wa Vifaa vya Mtaala wa somo la Kiswahili | 2 | 89.3 | 93.7 | Vizuri |
| | | 15 | 98.0 | | |
| 5. | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili | 4 | 97.7 | 90.4 | Vizuri |
| | | 6 | 83.1 | | |
| 6. | Stadi za Lugha | 3 | 86 | 86 | Vizuri |
| 7. | Ufahamu | 7 | 84.3 | 84.3 | Vizuri |
| 8. | Sarufi | 5 | 63.7 | 76.8 | Vizuri |
| | | 10 | 67.9 | | |
| | | 13 | 98.7 | | |
| 9 | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 8 | 48.8 | 48.8 | Wastani |
| 10 | Maandalizi ya Kufundishia Somo la Kiswahili | 16 | 43.3 | 43.3 | Wastani |

*Kiambatisho B*

**ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA MWAKA 2019 NA 2020**

